# AMRI ILIYOSAHAULIWA

## VITA JUU YA UTII WETU KWA KRISTO AU KWA MWANADAMU

**Danny Shelton**

Kusudi la kitabu hiki ni kutafuta kutoka katika Maandiko, "Je, kuna amri iliyosahauliwa?" Kama iko, basi maswali haya hayana budi kuulizwa, "Je, ni ipi?" na "Je, wale wanaodai kuwa Wakristo wangepaswa kuishika amri hii?"

•

Amri Kumi si Sheria ya Musa, wala ya Agano la Kale. Ni amri za Yesu. Zinatuonyesha tabia ya Mungu. Kwa maelfu ya miaka, mwanadamu amejaribu kuzichimba kwa patasi [zile mbao mbili za mawe za Amri Kumi] ili kuondoa maana yake na jinsi tunavyozihitaji. Lakini mkono wa Kristo umeilinda Sheria yake. Yeye aliishi ili kuzidhihirisha kanuni zake katika maisha yake, naye alikufa ili kuzihifadhi.

•

Mungu alimpa Musa Amri Kumi, lakini Wakristo wengi sana leo wanazishika tisa tu. Hivi kwa nini?

Hebu na tusome kwanza hizo Amri Kumi kutoka katika Toleo la Biblia la King James:

**Mungu akanena maneno haya yote akasema, Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila mimi.**

**Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.**

**Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.**

**Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.**

**Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako.**

**Usiue.**

**Usizini.**

**Usiibe.**

**Usimshuhudie jirani yako uongo.**

**Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako (Kutoka 20:3-17).**

Katika kuyachunguza mafungu haya, tunaona kwamba kwa mujibu wa amri ya nne, Mungu aliitenga, au aliitakasa, siku ya saba ya juma - siku tunayoiita Jumamosi. Kwa kweli, Mwanzo 2:2 husema kwamba wakati wa uumbaji Mungu "alistarehe [alipumzika]" katika siku ya saba "akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya." Basi, kutokana na kila kitu nilichopata kujifunza juu ya Mungu au hata kusikia juu yake, hakuna cho chote, hata kwa wazo la mbali, kinachodokeza kwamba yeye anachoka! Hapana budi alipumzika kwa sababu fulani, yaani, kuwa mfano kwetu sisi. Tunaona katikati kabisa ya ile amri ya nne, agizo la Mungu kwetu la kuitakasa siku ya saba ya juma - kumwabudu siku ile na kupumzika kwa kuacha kufanya kazi zetu za kawaida. Amri hii ya nne haiachi shaka lo lote kuhusiana nayo - yatupasa sisi kumtii yeye katika jambo hili sawasawa tu na vile tunavyopaswa kumtii katika zile amri nyingine tisa.

# Je hivi twaweza kuwa na hakika siku gani ya juma ni siku ya saba?

Swali kuu ambalo huenda tukawa nalo baada ya kuisoma amri ya nne ni hili: "Je, siku ipi ya juma ni siku ya saba?" Je, hivi kweli Jumamosi ni siku ya saba ya juma? Twajuaje? Labda kalenda zetu zote zimekosea. Pengine wakati umepotea au umeongezwa. Nimesikia kwamba kalenda nyingi kule Ulaya siku hizi zinasema kwamba Jumatatu ni siku ya kwanza ya juma, zinaifanya Jumapili kuwa siku ya saba. Hebu na tuyachunguze maswali haya.

Kwanza kabisa, hebu na tuone vile kisemavyo Kituo cha Uchunguzi cha Wanamaji cha Marekani (United States Naval Observatory) kilichoko kule Washington juu ya suala hili la kupotea au kuongezeka kwa wakati. Katika barua ya tarehe 12 Machi, 1932, Mkurugenzi, James Robertson, alisema hivi:

... Tumekuwa na wasaa wa kuchunguza matokeo ya kazi za mabingwa wa kupanga miaka na matukio, kamwe hatujamwona mmoja wao aliyepata kuwa na shaka lo lote juu ya kuendelea daima kwa mzunguko wa juma tangu muda mrefu kabla ya kuja kipindi cha Kikristo.... Hapajakuwako na badiliko lo lote katika kalenda zetu katika karne nyingi zilizopita ambalo limeathiri kwa njia yo yote ile mzunguko huo wa juma....

Kama uwezavyo kuona, kwa mujibu wa chanzo hiki, mzunguko wa juma bado ni ule ule kama ulivyokuwa miaka 2,000 iliyopita Kristo alipotembea hapa duniani. Pia, kutoka katika Maandiko twaweza kuona ya kwamba Yesu hakuwa na tatizo lo lote kujua siku ipi ya juma ilikuwa siku ya saba - yaani, siku ya ibada ya kila juma. Luka 4:16 asema, "Na siku ya Sabato [Yesu] akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake." Ulimwengu wote wa Kiyahudi katika siku zile za Yesu uliitakasa Sabato ya Mungu ya siku ya saba. Kwa kweli, Wayahudi wameendelea daima kuitunza Sabato ya siku ya saba.

Kama tunajiuliza iwapo kweli Jumamosi ndiyo siku ya saba ya juma, yaani, Sabato, basi, yatupasa kupanua mawazo yetu ili kufikia uamuzi kwamba Wayahudi wote ulimwenguni kote huenda wangeweza kwa njia fulani kuzichanganya siku za mzunguko wa juma tangu Yesu alipokuwapo hapa duniani. Na kama ingekuwa hivyo, basi, Wayahudi wa mahali mbalimbali ulimwenguni huenda wangekuwa wakitunza idadi yo yote ya siku zilizo tofauti. Badala yake, tunawaona wakiwa wameungana ulimwenguni kote juu ya suala hili lihusulo siku ipi ya juma ni Sabato ya siku ya saba.

Tunao ushahidi wa kibiblia pia, kwamba Jumamosi ndiyo siku ya saba ya juma, yaani, ndiyo Sabato Takatifu ya Mungu. Luka 23:54 husema kwamba siku ile aliyokufa Yesu "ilikuwa siku ya Maandalio, na Sabato ikaanza kuingia." Kisha Luka 24:1 husema kwamba siku ile aliyofufuka Yesu kutoka kaburini ilikuwa "siku ya kwanza ya juma." Kwa hiyo, kutoka katika Biblia tunao mfuatano wa siku tatu: siku ile iliyo kabla ya Sabato (siku aliyokufa Yesu), Sabato, na siku ya kwanza ya juma (siku aliyofufuka Yesu kutoka kwa wafu). Ulimwengu mzima unaitambua Ijumaa Kuu kama siku aliyokufa Yesu. Ulimwengu mzima unaitambua Jumapili ya Pasaka kama siku aliyofufuka Yesu. Na ile siku iliyo katikati ya Ijumaa na Jumapili, hivi ni siku gani? Ni Jumamosi. Na Agano Jipya linaiita siku hiyo kuwa ni "Sabato" (Luka 23:54). Mimi naamini kwamba tunayo maelezo ya kutosha kuweza kujua bila kuwa na shaka lo lote ya kwamba Jumamosi ya leo ni siku ile ile ambayo Biblia inaiita siku ya saba ya juma - yaani, Sabato Takatifu ya Mungu.

Pia ni jambo la kuvutia sana kuona kwamba mizunguko ya wakati inayowekewa mipaka yake hapa duniani inaamuliwa na elimu ya sayari. Siku inapimwa kwa muda inayochukua kuizunguka dunia, mwezi unapimwa kwa mzunguko wa mwezi ulio juu, na mwaka unapimwa kwa muda ambao dunia inachukua kulizunguka jua. Ni mzunguko wa juma peke yake ambao hautii nanga yake katika wakati unaopimwa kwa elimu ya sayari. Upimaji huo wa asili wa wakati unaweza kufuatiwa tu kwenda nyuma kwenye uumbaji wake Mungu wakati siku ya saba ilipotengwa kando kama Sabato.

# Je, Sabato hiyo bado ni sehemu ya mapenzi ya Mungu kwa Wakristo?

Sasa mimi nafikiri kwamba ungekuwa ni wakati unaofaa hapa kuangalia kwa nini Mungu aliwaamuru watoto wake kuitakasa siku ya saba ya juma. Kwa nini Mungu aliweke jambo linaloonekana kuwa halina maana katikati ya Amri Kumi? Na zaidi ya hayo, kwa nini amri ya nne ndiyo moja pekee katika zile kumi inayoanza na neno hili, "Ikumbuke"? Endapo Mungu alikuwa akienda kubadili au kuifutilia mbali amri ya nne kwa tarehe ya baadaye - kama Wakristo wengi wanavyoamini kwamba alifanya - je, ingeleta maana gani kwake kuanza amri ya nne kwa kusema, "Ikumbuke"? Kwa kweli, ingeonekana kwamba amri zile nyingine tisa zingepaswa kuanza na neno hili "Kumbuka" zaidi sana kuliko ile ya nne - kwa kuwa Wakristo wengi sana wanakubali kwamba hizi tisa bado zinawafunga watu wote leo na zitaendelea kuwafunga milele zote, wakati uo huo wanahisi kwamba amri ya nne iliondolewa. *Neno hili "Ikumbuke" linatuambia sisi kwamba Mungu alijua kwamba watu wangekuwa na matatizo na amri ile - ya kwamba wangejaribiwa kuisahau*.

Mungu anasema kwamba Sabato ni “agano la milele” na ya kwamba ni “ishara kati ya mimi na wana wa Israeli milele” (Kutoka 31:16,17). Baadhi ya Wakristo leo wanawezaje, basi, kusema kwamba Amri Kumi zilikuwa sehemu ya agano la kale na ya kwamba hazifai tena kwa watu wa Mungu?

Yanikumbusha juu ya wakati fulani ambapo familia yangu na mimi tulipoimba Jumapili moja asubuhi katika kanisa kubwa, lipendwalo na watu wengi, linalotunza siku ya Jumapili katika mji wa Tennessee. Baada ya ibada, mchungaji akaja kwangu na kuniambia, “Mtu fulani ameniambia hivi karibuni kwamba wewe ni Msabato. Je, ni kweli?

“Ndiyo,” nikamjibu.

Yule mchungaji akaendelea kusema, “Una maana kuniambia mimi kwamba wewe unaishi chini ya agano lile la kale? Nafurahi kusema kwamba mimi siishi tena chini ya lile agano la kale; niko chini ya neema!

Nakumbuka nilivyomtazama na kusema, “Sawa, hilo linasikika kuwa ni jema kwangu. Umenishawishi.” Kisha nikachukua sahani za sadaka ya Jumapili zilizokuwa karibu nami, halafu nikaanza kuondoka nazo.

“Lo! samahani, Ndugu Shelton,” akasema yule mchungaji, “lakini hiyo si sadaka yako! Hiyo ni sadaka ya kanisa. Tutakutumia hundi kwa fungu lako.”

“La,” nikajibu. “Nitachukua tu yote.”

Nilipoanza kutoka nje kwenda kwenye gari langu, mchungaji yule akanifuata kwa haraka kunijulisha mimi tena ya kwamba hii ilikuwa ni sadaka ya kanisa lake - si yangu mimi.

“Nafahamu,” nikamhakikishia. “Lakini kama Amri Kumi ziliondolewa pale Msalabani, basi, mimi kwa kweli siibi fedha yako kwa sababu hakuna neno lo lote liniambialo mimi kwamba ni vibaya kuchukua kitu fulani ambacho si mali yangu!”

Nilipomrudishia zile sahani za sadaka, yule mchungaji alielewa wazo langu na kupata muda wa kutafakari wazo lake la kutokuwa “chini ya sheria ile ya zamani.” Hebu sasa na tuangalie Biblia inavyoeleza maana ya dhambi. “Dhambi ni uvunjaji wa Sheria [Amri Kumi]” (1 Yohana 3:4, AJKK/HN). Hili ni mojawapo la mafungu rahisi sana kueleweka katika Biblia nzima. Endapo pasingekuwako na sheria, basi, pasingeweza kuwako dhambi yo yote.

Je! hivi kifo cha Yesu pale Kalvari kilizigongomea Amri Kumi msalabani? Hebu na tuone tena kile ambacho Biblia inasema juu ya somo hili. Yesu alisema, “Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati [sheria] au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza” (Mathayo 5:17). Ni jambo la kushangaza mno kwamba watu wengi sana, wakiwamo na wataalamu wa Biblia, wanajaribu kulilazimisha fungu hili kusema maneno fulani ambayo lenyewe halihalalishi kuyasema! Huwezi kulilazimisha fungu hili liseme kwamba kifo cha Yesu msalabani kiliifutilia mbali Sheria ya Amri Kumi. Hasha. Yesu asema hivi, “Sikuja kutangua, bali kutimiliza [au kuitekeleza].”

Sasa basi, *ni kweli* kwamba Yesu alizifutilia mbali sheria zile za kafara (ceremonial laws) alipokufa. Paulo asema kwamba Yesu alikwisha “kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani” (Wakolosai 2:14). Ni jambo zuri jinsi gani kujua kwamba kifo cha Yesu maana yake sisi hatuhitaji tena kuangalia damu ya wana-kondoo, au zile mbao mbili za mawe, au kujaribu kuwa wakamilifu kwa kutegemea matendo yetu wenyewe! Basi kwa kuwa Yesu amezichukua dhambi zetu mwilini mwake

mwenyewe katika msalaba ule wa Kalvari, haki yake inalipia fidia ya dhambi zetu kama tukiungama tu kwamba sisi ni wenye dhambi na kuomba msamaha wake. Biblia inasema kwamba "wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23). Pia inasema kwamba "tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9).

Sasa hebu na tuone kile kinachotokea hasa mchungaji anapotoa wito ili watu waje mbele. Kusudi lake ni nini? Si kitu kama yeye ni Mbaptisti, Mpresibiteri, Mpentekoste, Mmethodisti, au wa imani yo yote ile, kusudi lake ni kumfanya mtu yule aungame dhambi zake kwa Mungu na kisha amwombe Yesu aingie moyoni mwake ili apate "kuokolewa." Je, unaanza kulipata wazo hilo? **Endapo Sheria ya Mungu [ya Amri Kumi] iligongomewa msalabani, basi, kwa kweli hakuna haja ya kumtia moyo mtu fulani ili aombe msamaha, kwa sababu hakuna tena dhambi yo yote inayopaswa kusamehewa**.

Kwa nini? Ikumbuke tafsiri ya Biblia ya dhambi, ambayo ni "uvunjaji wa Sheria" (1 Yohana 3:4, AJKK/HN). Fuata sasa mkondo huu wa fikra. Kama sheria haipo tena, basi, hakuna dhambi tena, hivyo hakuna sababu ya kutubu dhambi zetu, halafu hakuna haja ya kuwa na Mwokozi, halafu hakuna haja ya kuwa na wachungaji. Na kama haja ya kuwa na wachungaji haipo, basi, hakuna haja ya kuwa na makanisa - na kadhalika. Sasa wazo hilo ni zito kweli! Hebu litafakari kwa dakika moja hivi, na kurudi nyuma na kuisoma tena aya ile na kuiacha izame kidogo ndani yako.

Kwa sasa, pengine unaanza kuuliza, "Kwa kuwa Biblia iko wazi mno hivyo kwamba Amri Kumi bado zinawafunga watu wote leo hii, basi, kwa nini makanisa mengi sana yanajaribu kutoa maelezo yanayozifutilia mbali?"

Tena, jibu lake ni rahisi sana. Kama tunakiri kwamba sheria ya Mungu ya Amri Kumi bado inawafunga watu wote leo, basi, hatuna budi kuikubali na kuitunza amri ile ya nne, tukitambua kwamba Jumamosi, siku ya saba ya juma, ndiyo Sabato ambayo Mungu, Muumbaji wa malimwengu, aliibarikia, aliitenga kando, aliitakasa, na kuifanya takatifu ili iwe siku yake ya ibada.

Ni nani athubutuye kukitenganisha kile alichokiunganisha Mungu? (angalia Mathayo 19:6). Iwe ni ndoa (ambayo Mathayo 19:6 yaongelea habari zake) au kiwe ni kile kitu kimoja cha pekee alichopata kukiandika Mungu juu ya jiwe kwa kidole chake mwenyewe - yaani, zile Amri zake Kumi - tunaonywa tusijaribu kukitenganisha kile alichokiunganisha Mungu. Lakini Wakristo kila mahali wangetaka sisi tuamini kwamba amri tisa tu zinawafunga watu wote leo. Wanaamini kwamba ni vibaya kuua, kuzini, kusema uongo, kuiba, ila wanasisitiza kwamba amri ya nne, iliyo na Sabato ya siku ya saba, imetengwa mbali na zile nyingine tisa na kusulibiwa juu ya msalaba wa Yesu.

Kwa kweli, kuna ulinganifu kadhaa wa kuvutia kati ya Ndoa na Sabato. Mambo hayo yote mawili yalianzishwa na Mungu katika Edeni katika juma lile la Uumbaji. Mungu aliyatakasa mambo yote mawili, ndoa na siku yake takatifu ya Sabato. Na kama vile isivyowezekana kwa mtu ye yote kuwatenganisha mume na mke waliounganishwa pamoja katika ndoa takatifu, ndivyo isivyowezekana kuitenga amri ya Mungu ya nne kutoka katika zile zilizobaki. **Mambo yote mawili, Ndoa na Sabato yamejengwa juu ya msingi wa kanuni ile ile moja - baraka na mamlaka ya Muumbaji aliyewapa wanadamu taasisi hizo zote mbili.**

Nimegundua kwamba haidhuru liwe jambo gani ninaloshughulika nalo katika maisha haya, sikuzote mimi nafanya maamuzi bora kabisa ninapojenga juu ya kanuni

fulani. Je, nina maana gani nisemapo "kanuni"? Kutenda kwa kufuata msingi wa kanuni maana yake ni kutotawaliwa na msisimko, hisia, maono ya moyoni, kutaka, au kuwa na shauku nyingi. Maana yake ni kujenga maisha yangu juu ya kile kilicho cha haki na kukataa kile kibaya kulingana na Neno la Mungu.

Hebu nikupe mfano huu. Wakristo wengi wanasema kwamba Mungu hajali mtu anatunza siku gani kama Sabato - licha ya Mungu kuitaja kabisa na kuiteua siku ya saba ya juma kama siku ya ibada. Hebu na tulinganishe kanuni iyo hiyo kuhusiana na wazo la ndoa na kuona mambo yatakavyokuwa. Na tuseme kwamba jioni moja wewe umekwenda kwenye mkutano wa maombi, na baada ya ibada kumalizika, unamtafuta mke au mume wako. Anaonekana amesimama karibu na marafiki zake sita. Unasema, "Mpenzi, wakati wa kwenda nyumbani umefika, lakini usiku wa leo nafikiri kwamba nitamchukua mmoja kati ya rafiki zako hao sita na kwenda naye nyumbani kukesha naye katika kitanda chetu. Najua tumeoana na ya kwamba ndoa yetu imetakaswa na Mungu, lakini kwa kuwa wewe uko pale na marafiki zako sita, sidhani kwamba wewe kweli unajali ni nani kati yao ninayelala naye, mradi tu ni mmoja wao!"

Nadhani wazo hilo linakuingia. Ukitaka kubaki ukiwa umeoa au umeolewa, nisingekutia moyo kujaribu kitu cha kipumbavu kama hicho! Kwanza kabisa, wewe usingeweza hata kutaka kufanya jambo hilo kwa sababu unampenda mke au mume wako. Pili, wewe unajua, kwa mujibu wa Neno la Mungu, kwamba kulala na mtu mwingine zaidi ya mke au mume wako ni dhambi. Ungekuwa unaivunja amri ile ya saba, isemayo, "Usizini" (Kutoka 20:14).

Kwa maana iyo hiyo, tunazini kiroho kwa kuivunja kwa makusudi amri ya Mungu ya nne na kuitunza siku nyingine ambayo haijawekwa, au haijatakaswa, au haijafanywa kuwa takatifu na Mungu. Mungu asema hivi, "Mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu" (Kutoka 20:5).

# Kuyaangalia Baadhi ya Mafungu Yanayotatiza

Ingawa hakuna mafungu yo yote katika Biblia yanayoonyesha kwamba Mungu aliibadili siku ya Sabato, yako mafungu machache tunayotaka kuyaangalia ambayo kwa juu juu yanaweza kuonekana kwamba yanaleta utata. **Twajua kwamba Biblia iliandikwa chini ya uvuvio wake Mungu**, **na kamwe haijikanushi yenyewe** - "**Kila andiko**, **lenye pumzi ya Mungu**" (2 Timotheo 3:16). Lakini baadhi ya mafungu yamewatatiza baadhi ya Wakristo walio wanyofu wa moyo walipokuwa wakijifunza juu ya suala hili la Sabato.

Kwa mfano, katika Wakolosai 2:13,14 mtume Paulo anasema hivi kumhusu Yesu: "Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu ..., [Yesu] aliwafanya hai pamoja naye akiisha kutusamehe makosa yote; akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani."

Wakristo wengi wanasonda kidole chao kwenye fungu hili kama ushahidi kwamba sheria ya Mungu ya Amri Kumi iligongomewa juu ya msalaba wa Yesu na kukoma wakati ule. Lakini tayari tumekwisha kuona kwamba Sheria ya Mungu ya Amri

Kumi itadumu milele. Kwa hiyo, ni sheria gani ambayo Paulo anaongelea habari zake? Ni sheria ipi iliyogongomewa juu ya msalaba wake Yesu?

Mafungu machache yanayofuata hutusaidia sisi kulijibu swali hilo:

"Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo" (fungu la 16 na 17).

Kwa hiyo, sheria, au ile hati ya kutushitaki kwa kuhumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu, ambayo Paulo anasema iligongomewa juu ya msalaba wa Yesu ilikuwa ni ile iliyoonyesha kivuli cha kazi ya Yesu ambayo angeweza kuifanya wakati wa kuja kwake kuishi katika dunia hii - yaani, kafara yake kama Mwana-Kondoo wa Mungu. Hizo, Paulo anaendelea kusema, ndizo sheria za kafara (ceremonial laws) ambazo Mungu aliwapa watu wake katika Agano la Kale ambazo zilihusu sadaka za vyakula na vinywaji, sikukuu za mwandamo wa mwezi, na "sabato" za kivuli kama vile Siku ya Upatanisho, Pentekoste, Sikukuu ya Vibanda (angalia Mambo ya Walawi 23:4-38). Kwa kweli, Mambo ya Walawi 23:39 kwa wazi kabisa huzitaja hizi "sabato" za kivuli (ambazo ziliweza kuangukia katika siku yo yote ya juma katika miaka mbalimbali) ambazo ni tofauti kabisa na Sabato ya siku ya saba ya kila juma ya amri ile ya nne.

Fungu jingine lililowatatiza baadhi ya Wakristo ni 1 Wakorintho 16:1,2. Paulo aliwaandikia maneno haya Wakristo waliokuwa kule Korintho:

"Kwa habari ya ile changizo (mchango) kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. **Siku ya kwanza ya juma** kila mtu kwenu na **aweke akiba kwake**, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja" (1 Wakorintho 16:1,2).

Wengine wamedhani kwamba Paulo alikuwa akiongea juu ya kukusanya sadaka kanisani katika siku ya kwanza ya juma na ya kwamba fungu hili, basi, lilionyesha kwamba Wakristo katika siku zake Paulo walikuwa wakiabudu siku ya Jumapili, yaani, siku ya kwanza ya juma. Lakini ukilisoma fungu hilo kwa makini, inakuwa dhahiri kwamba Paulo alikuwa akiwaambia waumini waliokuwa Korintho kukadiria nyumbani kwao siku ya Jumapili kiasi ambacho wangeweza kutoa kwa ajili ya mchango ule aliokuwa akikusanya kwa ajili ya waumini waliokuwa kule Yerusalemu. Walitakiwa ku"weka akiba kwa[o]" mchango ule ili uwe tayari kukusanywa na Paulo wakati atakapopitia Korintho akiwa njiani kwenda Yerusalemu. Hakuna kidokezo cho chote hapo kuonyesha kwamba Mungu alibadili siku ya ibada kuwa Jumapili.

Matendo 20:7 ni fungu jingine ambalo watu wengine hulitumia kujaribu kuthibitisha kwamba Kanisa lile la Kikristo la awali lilimwabudu Mungu katika siku ya Jumapili:

"Hata **siku ya kwanza ya juma**, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake."

Hapa tena, ukisoma kifungu hicho chote, utagundua kwamba ule ulikuwa ni mkutano wa aina yake uliokuwa umeitishwa kwa sababu Paulo alikuwa akipita katika eneo lile na kutaka kuonana na waumini aliokuwa amewaleta kwa Yesu katika safari zake za mwanzo za kimishonari. Wengine wamesema kwamba walikuwa wakishiriki Meza ya Bwana kwa sababu neno linasema kwamba wa"likutana ili kumega mkate." Ni dhahiri kabisa kwamba kile kilikuwa ni chakula chao cha kawaida na kwa vyo vyote vile, Matendo 2:46 husema kwamba Wakristo wale waumini wa mwanzo walimega mkate

"siku zote." Mara hii tena, hatuoni kidokezo cho chote kinachoonyesha kwamba Jumapili ni takatifu katika kanisa lile la Kikristo la awali.

# Mbona Wakristo wengi sana siku hizi Hawaijali Sabato ya Siku ya Saba?

Sasa kwa vile tumeonyesha kutoka katika Biblia kwamba Sheria ya Mungu ya Amri Kumi, ikiijumuisha ile amri ya nne, bado inaendelea kuwafunga wanadamu wote leo, waweza kuwa unashangaa kwa haki kabisa, na kusema, "Mbona Wakristo wengi sana – Waprotestanti na Wakatoliki - hawaitunzi Sabato takatifu ya Mungu ya siku ya saba?"

Kabla hatujalichunguza swali hilo, nataka jambo hili niliweke wazi kwa kusema kwamba mimi naamini Mungu anao wafuasi wake waaminifu katika kila kanisa. **Hatuokolewi kwa jina la dhehebu lililoandikwa juu ya mlango wa jengo la kanisa**. Naamini Mungu anamhukumu kila muumini peke yake moyoni mwake. Nawapenda watu wa imani zote - au hata wale wasio na imani yo yote. Yesu asema, "Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi" (Yohana 15:12). Kwa hiyo tunapozungumza juu ya Sabato ya Mungu, tunalazimika kushughulika na mafundisho ya kanisa na itikadi na mifumo - pande zote mbili, katika makanisa ya Kiprotestanti na ya Kikatoliki - lakini hatuihukumu mioyo ya watu.

Tunapoangalia ukweli unaoonyesha kwamba makanisa mengi sana ya Kikristo hayaitunzi Sabato ya Mungu ya siku ya saba, swali kuu ni hili: Kwa nini? Hii inaonekana kuwa ndiyo amri peke yake katika zile kumi ambayo inashambuliwa na mashirika ya makanisa ya Kikristo. Lazima pawe na sababu. Hapana budi kuna kitu ambacho Shetani hukichukia kweli kweli kuihusu hiyo amri ya nne. Je, ni kitu gani hicho? Hebu na tuisome tena ile amri ya nne:

"**Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa."**

Zingatia kwamba kuna kitu fulani cha maana sana kilichomo katika amri hiyo ya nne ambacho hakipatikani katika zile nyingine tisa. Amri ya nne inamtambulisha mwasisi wa amri zote kumi - Bwana ambaye "alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo." Sasa tunamjua huyo ni nani aliyeziandika zile Amri Kumi. Ni yule Mungu Muumbaji, Mungu wa malimwengu, yule MIMI NIKO mkuu! Sasa unifuate kwa karibu sana kwa dakika moja hivi.

Tukizichunguza hizo Amri Kumi, tutaona kwamba zimegawanyika katika sehemu mbili. Kwa kuzitii amri zile nne za kwanza tunaonyesha upendo wetu kwa Mungu. Tunapozitii zile za mwisho sita, tunaonyesha upendo wetu kwa mwanadamu mwenzetu. Kwa mfano, tunaonyesha utii wetu kwa Mungu kwa kutokuwa na miungu mingine mbele yake, kwa kutoisujudia miungu mingine, na kwa kutolitaja jina lake bure. Na

tunapoitunza ile amri ya nne - amri ya Sabato - tunaonyesha utii wetu kwa yule Mungu aliye Muumbaji pekee.

Amri ya nne ndiyo peke yake ituambiayo sisi ni Mungu yupi tunayemtumikia - ni yule Mungu ambaye "alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo" (Kutoka 20:11). Kama tukijaribu kuifutilia mbali amri ya nne, basi, hatujui hata ni Mungu gani tunayemtii. Nilikuwa India wakati fulani uliopita na kugundua kwamba kuna mamilioni ya miungu inayoabudiwa katika nchi ile. Mungu tunayemtumikia alituumba sisi; Yeye ndiye Muumbaji wetu. Ukweli huo - kuliko mwingine uwao wote - unamtofautisha Yeye na miungu hiyo yote iliyofanywa na wanadamu.

Za mwisho sita katika zile Amri Kumi huonyesha upendo wetu tulio nao kwa wengine. Kwa mfano, kama hatumwibii jirani yetu, kama hatuzini na mke wake, kama hatumshuhudii kwa uongo, na kadhalika, basi, tunadhihirisha kwa vitendo upendo wetu tulio nao kwa jirani yetu.

Amri ile ya nne, unaona, inao muhuri wa Mungu. Pasipo hiyo amri ya nne, tusingejua ni nani alikuwa ameziandika zile nyingine tisa. Fikiria kwa dakika moja hivi kwamba unasoma katika gazeti ya kuwa Marekani ndio kwanza imetangaza vita dhidi ya nchi nyingine! Swali la kwanza ambalo labda lingeweza kukujia mawazoni mwako lingekuwa ni hili, "Nani asemaye hivyo?" Hata hivyo, kuna karibu Wamarekani 300,000,000. Ye yote kati yao angeweza kutangaza vita dhidi ya nchi nyingine, lakini hilo lisingekuwa na maana, isipokuwa kama mtu fulani mwenye mamlaka angetia sahihi katika tangazo la vita baada ya Bunge la Marekani kuchukua hatua ile. Muhuri wake una sehemu kadhaa: (1) jina lake – George W. Bush; (2) cheo chake - Rais; (3) eneo analotawala au himaya yake - Marekani. Uwe na hakika kwamba kama George W. Bush, Rais wa Marekani, akitia sahihi yake katika tangazo la vita, basi Amerika imejiingiza kweli kweli katika vita hiyo!

Muumbaji wetu Mungu anao muhuri wake katika amri hiyo ya nne: (1) Jina lake - "BWANA, Mungu wako"; (2) Cheo chake - Muumbaji; (3) Eneo lake au himaya yake - "mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo."

Kumbuka, Biblia inasema kwamba kulikuwa na vita mbinguni. "Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda" (Ufunuo 12:7,8). Kwa nini vita vilitokea kule mbinguni? Kwa sababu Shetani alimwonea wivu Mungu. Alisema, "Nitafanana na yeye Aliye juu" (Isaya 14:14). Aliweza kuwashawishi theluthi moja ya malaika ili wamfuate yeye (angalia Ufunuo 12:4).

**Pambano kuu kati ya Kristo na Shetani linaendelea kupamba moto leo - isipokuwa Shetani sasa anafanya kazi kuwafanya wanadamu watoe utii wao kwake badala ya kuutoa kwa Mungu**. Shetani anajua kwamba yeye na malaika zake waovu wamepotea, lakini anataka kumdhihaki Mungu mbele ya malimwengu yote kwa kutuangamiza sisi, tulio viumbe vyake Mungu (angalia Yohana 10:10). Bado yeye anataka kufanana na Mungu Aliye juu. Kwa hiyo anawarubuni wanadamu utii wao kwa kuwafanya wale walio mawakala wake wazibadili Amri Kumi za Mungu na kwa njia hiyo kuyadanganya mataifa yote ili yamfuate yeye badala ya kumfuata Mungu Muumbaji wa malimwengu.

Kaka na Dada zangu, hoja yenyewe haihusu siku tu; inahusu **utii** wetu. Swali lenyewe ni hili: Je, tutamtumikia nani? Je, tunampenda Mungu kiasi cha kutosha kumtumikia yeye na kuzishika amri zake kwa ukamilifu - ikiwamo na ile ya nne? Au

sisi tutamtumikia Shetani na kumwabudu yeye katika siku yake ya bandia iliyowekwa na wanadamu? Je, jambo hili linawezekana? Hebu na tuone Biblia inayo maneno gani ya kutuambia. "**Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu**" (Marko 7:7). Kwa kweli, ukilisoma fungu hilo kwa karibu sana, utaona kwamba Yesu anatabiri kwamba hilo litatokea. Tena, si juu ya siku tu; bali ni juu ya utii wetu.

Angalia pia Yakobo 2:10: "**Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote**." Je, ni sheria ipi ambayo Yakobo anaongelea habari zake? Ni Sheria ya Amri Kumi ambayo Mungu aliiandika juu ya mbao mbili za mawe kwa kidole chake mwenyewe; angalia fungu linalofuata: "**Kwa maana yeye aliyesema, Usizini, pia lisema, Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria**" (Yakobo 2:11). Hebu tafakari maneno hayo. Nadhani sisi sote tunaweza kukubaliana kwamba Yesu ndiye "jiwe kuu la pembeni." Viumbe vyote vinalitegemea jiwe hilo la pembeni. Jiwe hilo ambalo juu yake Mungu aliiandika Sheria yake linamwakilisha Yesu mwenyewe - Jiwe Kuu la Pembeni. Sheria ya Amri Kumi si cho chote ila ni nakala halisi ya tabia yake Kristo. Sheria hiyo ya Amri Kumi ni Neno lake Mungu. Yohana asema hivi, "Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu" (Yohana 1:14). Hebu fikiria hilo!

Yesu, Jiwe Kuu la Pembeni, alimpa Musa zile Amri Kumi zilizoandikwa juu ya mbao zile za mawe zilizomwakilisha yeye mwenyewe. Biblia inaandika kumbukumbu isemayo kwamba Musa alikasirika alipouona uovu wa watu wale, akazitupa chini zile mbao za mawe na kuzivunja (angalia Kutoka 32:19). Lakini, je! kitendo kile kiliifutilia mbali Sheria ya Mungu? La. Biblia inaandika kumbukumbu isemayo kwamba Mungu alimpa mbao nyingine mbili zilizokuwa na zile Amri Kumi. Hizi ziliwekwa ndani ya sanduku la agano katika patakatifu na hatimaye zilifichwa wakati ule Waisraeli walipokwenda uhamishoni. Kuna ishara fulani zinazodokeza kwamba mbao hizi za mawe zenye sheria iliyoandikwa juu yake na Mungu mwenyewe zitaonyeshwa kwa ulimwengu mzima kwa wakati aliouweka Mungu.

Kwa njia ile ile, mwili wa Yesu ulipondwa-pondwa kwa ajili yetu alipokufa juu ya msalaba ule (angalia 1 Wakorintho 11:24). Kama ilivyokuwa kwa zile mbao za mawe zilizovunjika, mwili wa Yesu uliopondwa-pondwa ndivyo ulivyokuwa hauwezi kuifutilia mbali sheria ya Mungu, bali uliitimiza (angalia Mathayo 5:17). Halafu, baada ya kifo chake, Yesu alipaa kwenda mbinguni kutuombea sisi mpaka utakapotimia wakati uliowekwa atakaporudi, na dunia yote itakapomwona na kujua kwamba yeye ndiye Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana. Bwana asifiwe!

Je, huoni kwamba ni jambo la ajabu kwamba Mungu alitupenda kiasi cha kutosha hata kutuwekea kando siku ya masaa ishirini na manne kila juma ili sisi tuweze kuutumia muda wetu pamoja naye? Ni kumbukumbu ya kila juma inayoonyesha kwamba anatupenda, wala hajatusahau. Rafiki yangu mmoja anazitaja Amri Kumi kama "Ahadi Kumi." Ni njia ya ajabu jinsi gani ya kuzifafanua! Biblia inasema kwamba yatupasa kuvaa silaha zote za Mungu (Waefeso 6:11). Tunapozivaa - yaani, tunapoivaa tabia ya Mungu, yaani, Amri zake Kumi, yeye anatuahidi kutupa ushindi dhidi ya yule mwovu. Kwa mfano, hatutapoteza uwezo wa kujitawala kiasi cha kumwua mtu fulani. Hatutaangukia katika wizi au uzinzi. Anatuahidi sisi kutupa ushindi dhidi ya kusema uongo au kutamani. Ni upendo ulioje huo! Wimbo wa zamani unasema hivi, "Mwokozi

wa ajabu ni Yesu Bwana wangu, ni Mwokozi wa ajabu kwangu." Maneno ya kweli zaidi ya hayo hayajanenwa kamwe.

# Sabato Inavyomaanisha Kwangu Mimi Binafsi

Tumekwisha kuona kitu fulani ambacho Biblia inasema juu ya Sabato ya Mungu ya siku ya saba na umuhimu wake. Basi, kabla hatujaendelea mbele kuangalia vipengele vingine vya somo hili na umuhimu wake kwa nyakati hizi tunazoishi, ningependa kueleza kwa kifupi Sabato inavyomaanisha kwangu mimi kwa mtazamo wa kibinafsi.

Kwangu mimi, Sabato hii ya Bwana ya siku ya saba ni wakati unaovutia sana wa kila juma. Ni kimbilio langu mbali na matatizo yangu ya kila siku katika maisha haya. Katika muda wa Sabato naona kama nimeinuliwa juu katika ulimwengu wa roho na kushirikiana kwa karibu sana na Mungu. Katika kila siku saba Sabato hunikumbusha mimi ya kwamba Yesu ananipenda na ya kwamba hajanisahau. Inanikumbusha kwamba Yesu anakuja tena upesi sana katika dunia hii kuja kunikomboa kutoka katika ulimwengu huu uliolemewa na maradhi ya dhambi. Sabato ya siku ya saba ni agano lake Mungu - au mapatano yake - pamoja nami ya kwamba mimi ni wake na yeye ni wangu katika umilele wote. Angalia kile alichosema Mungu huko nyuma katika siku za Wana wa Israeli: "Hakika mtazishika Sabato zangu, kwa kuwa ni ishara kati ya mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa mimi ndimi BWANA niwatakasaye ninyi" (Kutoka 31:13). Fungu la 17 linasema kwamba Sabato ni ishara kati ya Mungu na watu wake "milele."

Siku ya Sabato naweza kuyaacha nyuma yangu masumbufu yangu ya kila siku. Shughuli zangu zote za kazi au biashara - yaani, nani ananidai, na nani namdai, kiasi gani kiko au (hakiko) kule katika Akaunti yangu ya Benki, mambo haya yote yanaweza kutoweka kwa masaa ishirini na manne. Sihitaji kuwa na wasiwasi juu yake au kuyashughulikia. Hebu nikuambie, ni jambo la kushangaza kujitenga mbali na shughuli zote za kununua na kuuza. Bwana anajua kwamba hatuwezi kukaza mawazo yetu juu ya uhusiano wetu naye kama tunashughulika na mambo yetu ya kila siku ya maisha haya. Ndiyo maana anatuambia kuepukana na kufanya kazi siku ya Sabato, au kuachana na kununua na kuuza vitu.

"BWANA akaniambia hivi, Enenda ukasimame katika lango la wana wa watu hawa, waingiapo wafalme wa Yuda, na watokeapo, na katika malango yote ya Yerusalemu, ukawaambie, Lisikieni neno la BWANA, enyi wafalme wa Yuda, na Yuda wote, nanyi mwingiao kwa malango haya; BWANA asema hivi, Jihadharini nafsi zenu, msichukue mzigo wo wote siku ya Sabato, wala msiulete ndani kwa malango ya Yerusalemu; wala msitoe mzigo katika nyumba zenu siku ya Sabato, wala msifanye kazi yo yote; bali itakaseni siku ya Sabato, kama nilivyowaamuru baba zenu; lakini hawakusikiliza, wala hawakutega masikio yao, bali walifanya shingo zao kuwa ngumu, ili wasisikilize wala wasipokee mafundisho. Na itakuwa, kama mkinisikiliza mimi kwa bidii, asema BWANA, msiingize mzigo wo wote kwa malango ya mji huu siku ya Sabato, bali mkiitakasa siku ya Sabato, bila kufanya kazi yo yote siku hiyo; ndipo watakapoingia wafalme na wakuu kwa malango ya mji huu; wataketi katika kiti cha enzi

cha Daudi, na kupanda magari na farasi, wao, na wakuu wao, watu wa Yuda, na wenyeji wa Yerusalemu;  na mji huu utakaa hata milele" (Yeremia 17:19-25).

Bwana anajua pia kuwa tunahitaji pumziko la kimwili pamoja na pumziko la kiakili katika siku ya Sabato.  Nashukuru kwamba anatuambia sisi katika amri ya nne kuacha kufanya kazi zetu zote za sulubu na za kawaida kwa masaa ishirini na manne ya Sabato.  Sayansi ya Kiganga itathibitisha kwamba mtu ye yote anayefanya kazi siku saba kwa juma atajiteketeza kwa haraka kuliko mtu yule anayefanya kazi siku sita kama Mungu alivyoamuru  -  na kupumzika siku ya Sabato.

Wakati mwingine watu wanafadhaika juu ya ipi ni kazi na ipi si kazi siku ya Sabato.  Kwa maoni yangu,  mijadala ya jinsi hii inaishia katika mgawanyiko wa kutetea utunzaji wa sheria ili kupata wokovu.  Ni rahisi sana kuyachambua mambo hayo, kwa kadiri niwezavyo kuona mimi.  Mungu alitoa kielelezo kwa ajili yetu sisi.

"Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote.  Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya;  akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya.  Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya" (Mwanzo 2:1-3).

Je, ni kazi gani aliyoiacha na kupumzika?  Ni kazi ile ya kuiumba dunia, kusema kweli.  Lakini hebu nikuulize swali jingine:  Je, hivi Mungu anaacha kutenda kazi kwa ajili yetu siku ya Sabato?  Je, Yesu anaacha kutuombea siku ya Sabato?  Kusema kweli, haachi!  Biblia inatuambia kwamba "**Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu**, **si mwanadamu kwa ajili ya Sabato**" (Marko 2:27).  Je, hivi Mungu alipumzika katika Sabato ile ya kwanza mwisho wa juma lile la Uumbaji kwa sababu alikuwa amechoka? La.  Alipumzika kuweka kielelezo kwa ajili yetu sisi kukifuata.  Vilevile, siku ya Sabato tunapaswa kujitenga mbali na kazi zetu za kila siku kwa maana ya kuzifanya kazi zile tunazofanya katika siku zile nyingine sita za juma.  Lakini tusingeiruhusu Sabato kutuzuia tusifanye mapenzi ya Mungu katika kipindi cha saa zake.  Tusiwe kama wengine wanaoogopa kwamba hawataweza kuitunza Sabato kwa usahihi kiasi kwamba hawaendeshi gari, hawatembei umbali wa maili moja, wala hawamsaidii jirani mwenye shida katika siku ya Sabato.

Napata amani nyingi moyoni mwangu kwa kuitunza Sabato wakati ninapokaza mawazo yangu juu ya uhusiano wangu na Mungu na uhusiano wangu na wanadamu wengine.  Kwa maneno mengine,  najitahidi kuitumia Sabato kwa ajili ya huduma.  Sivuti kiti cha starehe na kukaa tu siku nzima ya Sabato.  Wala siitumii Sabato kwa kulala kitandani.  Najitahidi kukaza mawazo yangu juu ya kuwasaidia wengine.

Waweza kuuliza, "Unafanyaje hivyo kimatendo?"  Hapa kuna baadhi ya mapendekezo ambayo kwangu yamefanya kazi.

Lakini usiende kanisani ukitazamia kwamba kila mmoja atakuhudumia wewe katika mahitaji *yako*.  Panga ili uwe mbaraka kwa wale wanaokuzunguka.  Shiriki katika Shule ya Sabato.  Kama huwezi kufundisha darasa, basi, msaidie mwalimu kwa kutoa mchango wako wa mawazo katika mjadala wa lesoni.  Kama wewe huwezi kuimba, unaweza kutoa ushuhuda wako katika kipindi cha kumsifu Bwana.  Kama una aibu mno kufanya hivyo, unaweza kukusanya sadaka, unaweza kusaidia kuendesha mtambo wa sauti, au kusaidia kwa njia nyingine ukiwa umejificha nyuma ya shughuli zinazoendelea. Unaweza kuleta chakula kwa ajili ya chakula cha mchana baada ya ibada.  Kama kanisa

lako halina chakula cha mchana, basi, mkaribishe mtu fulani nyumbani kwako kwa chakula cha mchana - hasa mtu fulani mwenye shida. Kwangu ni muhimu kwenda kanisani sio tu kupokea mbaraka, bali kuwa mmoja aletaye mbaraka kwa wengine.

Sabato ya Mungu ya siku ya saba ni wakati mzuri pia wa kutumia na familia yako - yaani, unapokuwa kanisani na sehemu iliyobaki ya siku hiyo. Takwimu za sasa zinaonyesha kwamba mzazi wa kawaida anatumia dakika chache tu kwa siku pamoja na watoto wake. Sabato alasiri ni wakati mzuri kwa familia nzima kwenda matembezini kuangalia viumbe vya asili. Angalia kila upande, kisha furahia kuwa katika maeneo ya nje. Mimi nina bahati sana kulelewa na wazazi walionifundisha ukweli kuhusu Sabato ya Mungu ya siku ya saba. Baadhi ya kumbukumbu zangu tamu sana za utotoni sikuzote huhusiana na muda ambao familia yangu ilitumia pamoja wakati wa Sabato Takatifu ya Mungu.

Kugawa vitabu vya injili ni njia nyingine kuu ya kuitumia Sabato pamoja na familia yako. Kumbuka, Sabato haituhusu sisi. Inahusu uhusiano wetu na Mungu. Ni nafasi nzuri ya kuwatumikia wengine. Maandiko yanatuambia kwamba Yesu alitumia muda mwingi wa Sabato kuponya wagonjwa na kuwahudumia wengine. Mimi naamini watakuwako watu wengi kule mbinguni kwa sababu mtu fulani aliwajali kiasi cha kutosha kutumia muda wake na juhudi yake kuwaleta kwa Yesu kwa njia ya vitabu. Na, kusema kweli, Sabato ni wakati wa ajabu kwa maombi ya mtu binafsi na kujifunza Maandiko kwa sababu kadiri tunavyomkaribia zaidi Yesu, ndivyo kadiri tutakavyotaka kuwaeleza wengine habari zake.

# Je, Hivi Mungu Anajali?

Si ajabu, basi, kwamba Shetani anataka Wakristo waisahau amri ya Sabato - amri ya pekee ambayo Mungu alisema kwa dhahiri kwamba sisi tu"ikumbuke." Kutoijali amri hiyo ya nne huyageuza macho yetu kutoka kwa Mungu pekee wa kweli awezaye kutupa sisi ushindi dhidi ya dhambi na kufanya uwezekano uwepo kwetu wa kumshinda yule joka wa zamani, yaani, Shetani.

Ikielezwa kwa njia rahisi sana, ni kama hivi: Kwa kujaribu kuibadili Sabato kutoka siku ya saba ya juma, ambayo Mungu wetu Muumbaji aliiweka, kwenda Jumapili, siku ya kwanza ya juma, Shetani anauondoa "muhuri" wa Mungu, yaani, anaondoa mamlaka yake duniani. Kwa kuitunza Sabato ya uongo, tunamsujudia Shetani, jambo ambalo amelitaka tangu dhambi ilipoanza kule mbinguni kwa miaka 6,000 hivi iliyopita.

Je, hivi Mungu anajali kweli? Je, hivi siku hiyo ina maana kwake? Hebu na tuangalie katika 1 Yohana 2:4. "Yeye asemaye, Nimemjua [Yesu], wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake." Neno hili "amri" lililotumika katika lugha ya asili (*entolai*) linahusu maagizo au sheria za Yesu alizozifundisha na kuishi kwazo na kwa hakika hizo hujumuisha Amri Kumi. Biblia inatoa mifano kadhaa ya Mungu alivyowakataa wale walioshindwa kuzifuata amri zake. Hebu na tuangalie michache tu.

Kaini na Habili wote wawili walileta sadaka zao kwa Mungu. Habili alileta mwana-kondoo kama Mungu alivyokuwa amemwagiza. Lakini Kaini alileta matunda na mboga za majani kutoka katika ardhi. Alishindwa kufuata maagizo ya Mungu. Mungu alimkubali Habili na sadaka yake, lakini alimkataa Kaini na sadaka yake.

Vilevile, Uza alinyosha mkono wake ili kulizuia sanduku la agano lisianguke chini, huku akiwa anajua kwamba Mungu alikuwa ameamuru kwamba mtu awaye yote asiliguse sanduku lile takatifu lililohusiana na pataktifu. Huenda aliwaza kwamba Mungu alikuwa hajali sana. Lakini Uza alilipa kwa kupoteza uhai wake kwa kiburi chake (2 Samweli 6:6,7). Mungu ana maana na kile asemacho!

Hata Musa mwenyewe, mtu wa imani kama vile alivyokuwa, alikuwa na nyakati za udhaifu na kushindwa. Wana wa Israeli walipokuwa wakifa kwa kiu jangwani, Mungu alimwambia Musa kuuambia mwamba na maji yangebubujika kwa nguvu kwa wingi kwa ajili ya watu wale na wanyama wao. Lakini Musa alivunjika moyo mno kutokana na malalamiko ya watu wale hata akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake - kama alivyokuwa amefanya mara ya kwanza. **Maji yalitoka kwa wingi na kububujika**, **bali Mungu hakupendezwa kwa kuwa Musa alikuwa hajafanya kile alichomwambia afanye**. Musa ilimbidi alipe kwa dhambi yake kwa kukosa kuingia katika ile Nchi ya Ahadi (angalia Hesabu 20:7-12).

Huonekana kama ni jambo dogo tu - kuupiga mwamba badala ya kuuambia. Lakini kwa kweli halikuwa suala la kama Musa aliupiga ule mwamba au aliuambia. Lilikuwa suala la utii. Je, angemtii Mungu au la? Hiyo ndiyo hoja yenyewe. Jumamosi au Jumapili - siku ya saba ya juma au siku ya kwanza. Kwa kweli, hili si suala la siku. **Ni suala la utii**. Je, tutamtii Mungu au la?

# Jinsi Badiliko hilo Lilivyotokea

Kama kweli Sabato ya Mungu ni Jumamosi, siku ya saba ya juma, lilitokeaje badiliko hilo? Kwa nini ulimwengu wa Kikristo ungetaka kuiweka Jumapili mahali pa Sabato ya Mungu ya siku ya saba? Hilo ni swali zuri - ni moja ambalo watu wengi sana wanauliza wanapogundua kwa mara ya kwanza kwamba Jumamosi ndiyo Sabato ya Biblia.

Kwanza, tungezingatia kwamba kama Jumapili si Sabato ya Biblia, basi, hilo ni kosa. Na Paulo aliwaonya viongozi wa Kikristo kule Efeso kwamba makosa yangeingia kwa siri ndani ya kanisa:

"Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao" (Matendo 20:29,30).

Historia ya kanisa inaandika kwamba, kwa bahati mbaya, jambo hilo lilikuja kutokea. Kwa haraka sana, kanisa lile la awali likajikuta limenaswa katika makosa mengi ya mafundisho ya dini. Paulo aliliambia kanisa lile la Thesalonike kwamba roho ya chuki dhidi ya sheria za Mungu ingetokea ndani ya kanisa, na ya kwamba, kwa kweli, ilikuwa tayari imeanza kufanya kazi yake (angalia 2 Wathesalonike 2:3-7). Sabato ilikuwa ni mojawapo ya Sheria za Mungu ambayo iliathirika sana katika historia ya kanisa la mwanzo na kupitia katika karne nyingi zilizofuata. Ingawa baadhi ya Wakristo walibaki wakiwa waaminifu kwa siku hiyo ya Mungu ambayo kwa gharama kubwa alikuwa ameitenga kando katika Neno lake, sehemu kubwa sana ya Wakristo waliiacha taratibu Sabato ya siku ya saba ya kibiblia na kuitunza siku ya kwanza ya juma. Ni kitu gani kilichowashawishi kufanya badiliko kama hilo licha ya kuwako amri dhahiri ya

Mungu? Mambo mawili hasa yalipelekea kanisa kuiweka siku ya kwanza ya juma badala ya ile ya saba.

*Kuwachukia Wayahudi*. Kulikuwa na mjadala mkali katika kanisa la Agano Jipya kuwahusu Wakristo wa Mataifa endapo wangepaswa kuzitii taratibu zote za ibada na sikukuu za dini ya Kiyahudi. Hiki kilikuwa kipengele cha kwanza kilicholipeleka kanisa mbali na Sabato ya Mungu. Wakristo wa kwanza walikuwa Wayahudi. Kwa kawaida, waliendelea na desturi nyingi za Agano la Kale ambazo walikuwa wamezoea kuzifuata. Kundi moja ndani ya kanisa lilidai kwamba waongofu wa Mataifa wafuate desturi zile zile, wakati kundi jingine lilisisitiza kwamba hilo lilikuwa si jambo la lazima - na kusema kweli, halikuwa la lazima.

Hatimaye, kanisa liliamua kuwapa uhuru watu wale wa Mataifa. Lakini hoja yenye nguvu iliyotumika dhidi ya taratibu za ibada za Agano la Kale - kama vile tohara na dhabihu za patakatifu - hazikueleweka dhahiri wakati ulipozidi kusonga mbele. *Kila kitu* kilichohusiana na Wayahudi kikawa cha kutiliwa mashaka. Na kwa kuwa Wayahudi waliitunza Sabato ya siku ya saba, Wakristo wakaja kuidharau siku hii kama walivyofanya kwa desturi nyingine walizozifikiria kuwa zilikuwa za Kiyahudi hasa. Kanisa la Kikristo lilipokua, lilizidi sana kutaka kujitenga mbali na jumuia ya Kiyahudi ambayo kutokana nayo lilikuwa limetokea.

*Injili*. Kipengele cha pili kilikuwa ni ile hamu yao ya kuwavuta wapagani kuingia kanisani. Wapagani walipoongolewa, walileta pamoja nao baadhi ya mawazo yao ya zamani. Dini nyingi sana za kipagani tayari zililiheshimu jua katika siku ya kwanza ya juma. Kwa kweli, ndivyo siku hiyo ilivyopata jina hili la *Sunday* [Siku ya Jua]! Viongozi wa kanisa wakaanza kuwaza kwamba ingekuwa ni rahisi zaidi kuwapata waongofu wa kipagani kuingia kanisani kama wangeweza kuendelea kuabudu katika siku ile ambayo wao walikuwa wamezoea kuiheshimu.

Kwa hiyo kutaka kuepuka kujifananisha na Wayahudi, pamoja na hamu ya kuufanya Ukristo uwe wa kuvutia zaidi kwa wapagani, mambo hayo yalifanya iwe rahisi kwa kanisa lile la mwanzo kuipa umaarufu wa pekee siku ile ya kwanza ya juma. Ufufuo wa Yesu katika siku ile uliandaa sababu ya kutumia.

Haya ni baadhi ya mambo tunayoyaona katika historia ya kanisa la Kikristo katika nyakati zile za mwanzoni kwa ajili ya kuitukuza zaidi Jumapili na Jumamosi kupoteza umaarufu wake. Kanisa lile la mwanzo la Kikristo - shirika tunalolijua sasa kama Kanisa Katoliki la Roma - likaendelea kupendwa na watu wengi sana na kuwa na nguvu, halafu likajiunga na serikali. Chini ya uongozi wa kanisa, Mtawala wa Dola ya Kiroma, Konstantino, katika mwaka wa 321 B.K. alitoa amri ya kwanza iliyowataka watu kuacha kufanya kazi zao na kwenda kuabudu siku ya Jumapili.

# Ni Nani Anayedai Kuibadili Sabato Kwenda Jumapili?

Kwa kweli, Mungu aliona mapema kwamba badiliko hili lingeweza kutokea ndani kabisa ya kanisa. Je, hivi ulijua kwamba kupitia kwa nabii Danieli, Biblia inatabiri kwamba mamlaka moja ya kidini ingeazimu kweli kweli kubadili Sheria ya Mungu? Utabiri huu uliandikwa katika karne nyingi za nyuma kabla Yesu hajazaliwa kule Bethlehemu. Hebu na tuuangalie utabiri huu na kuona jinsi “badiliko” hilo lilivyotokea.

Akizungumza juu ya mamlaka hii aliyoiona katika maono, Danieli anasema, "**Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu**, **naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu**; **naye ataazimu kubadili majira na Sheria**" (Danieli 7:25). Zingatia kwamba mamlaka hii anayoongelea habari zake itakwenda kinyume na Mungu, "Aliye juu," na kujaribu kubadili "majira na Sheria" zake. Twajuaje kwamba Danieli alikuwa akisema kwamba mamlaka hii ingebadili "majira na Sheria" za Mungu? Zingatia kwamba kifungu hicho cha maneno kinaonekana katika orodha ya mashtaka ambayo Mungu analeta dhidi ya mamlaka hiyo: ina hatia ya makufuru, kutesa na kuwaua watu wa Mungu, na ***kubadili "majira na Sheria."*** Mamlaka za kibinadamu zina haki kamili kubadili desturi na sheria zilizowekwa na wanadamu. Kwa hiyo, kwa kuwa Mungu anazingatia kwamba kile ambacho mamlaka hii imekifanya ni kibaya mno, basi, ***hapana budi hayo ni "majira na Sheria" za Mungu - si zile zilizowekwa na wanadamu - ambazo mamlaka hii imefanya jaribio la kuzibadili***.

Haya basi! Ni sheria ipi ya Mungu inayoshughulika na majira? Ni moja tu kati ya zile Amri Kumi za Mungu ihusuyo majira [wakati] - ni ile amri ya nne inayotaja waziwazi kwamba siku ya saba ya juma ni Sabato Takatifu ya Mungu. Danieli alisema kwamba mamlaka hii ingefanya jaribio la kubadili Sheria ya Mungu inayohusu majira, yaani, Sabato. Je, kuna mamlaka yo yote ya kidini duniani leo inayodai kwamba imebadili siku ya Sabato ya Bwana? Kwa kweli, ipo. Hebu na tuyaangalie baadhi ya madondoo kutoka kwa mamlaka hii inayodai kwamba tayari imefanya kitendo kama hicho:

"Kanisa Katoliki kwa zaidi ya miaka elfu moja kabla ya kuwako kwa Mprotestanti mmoja, kwa sababu ya utume wake wa Kimungu, lilibadili siku kutoka Jumamosi kwenda Jumapili.... Sabato ya Kikristo, kwa hiyo, *mpaka leo hii* ni mtoto anayekubalika wa Kanisa Katoliki ... bila ya kuwako neno lo lote la kupinga kutoka kwa ulimwengu wa Kiprotestanti." (*The Christian Sabbath*, toleo la 2, "The Catholic Mirror," Baltimore, 1893.)

S. *Siku ya Sabato ni ipi?*

J. Jumamosi ndiyo siku ya Sabato.

S. *Kwa nini tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi?*

J. Tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu Kanisa Katoliki lilihamisha ibada kutoka Jumamosi kwenda Jumapili. (Peter Geiermann, *The Convert's Catechism of Catholic Doctrine*, St. Louis, 1957).

S. *Je, unayo njia nyingine ya kuthibitisha kwamba Kanisa [Katoliki] lina mamlaka ya kuweka sikukuu zinazoshikwa kama amri?*

J. Lisingekuwa na mamlaka kama hiyo, lisingeweza kufanya kile ambacho wanadini wote wa siku hizi wanaafikiana nalo; - lisingeweza kuweka utunzaji wa Jumapili, siku ya kwanza ya juma, mahali pa utunzaji wa Jumamosi, siku ya saba, badiliko ambalo halina mamlaka ya Maandiko. (Stephen Keenan, *A Doctrinal Catechism*, New York, 1876).

"Unaweza kusoma Biblia toka Mwanzo hadi Ufunuo, nawe hutaukuta mstari hata mmoja unaoamuru kuitakasa Jumapili. Maandiko yanakazia amri ya kidini ya kuitunza Jumamosi, siku ambayo sisi hatuitakasi kamwe." (Cardinal Gibbons, *The Faith of Our Fathers*, uk. 111).

"Ni kweli Kanisa Katoliki linadai kwamba badiliko hili [la Sabato kutoka Jumamosi kwenda Jumapili] lilikuwa ni kitendo chake.... Na kitendo hiki ni **alama ya mamlaka yake** ya kikanisa." (Barua ya H.F. Thomas, chancellor of Cardinal Gibbons).

Tafadhali kumbuka kwamba hizo si semi zangu. Hizo ni madondoo kutoka katika vitabu na wawakilishi wa Kanisa Katoliki, wakikiri bila kusita kwamba kitendo hiki cha kuibadili amri ya Sabato ya Mungu kilifanywa kwa mamlaka ya Kanisa Katoliki la Roma peke yake. Sasa, tafadhali, usinielewe vibaya. Hapa hatuzungumzi juu ya mtu mmoja mmoja; tunazungumza juu ya taasisi ya kidini na mifumo yake. **Mungu anao wafuasi wake waaminifu katika kila kanisa na kila dhehebu - pamoja na Kanisa Katoliki la Roma**. Lakini Neno la Mungu lisemapo kwamba mamlaka ya kidini itatokea ambayo itafanya jaribio la kubadili sheria za Mungu zinazohusu majira (wakati), na Kanisa Katoliki linaposema waziwazi na bila kigugumizi cho chote kwamba tayari limefanya badiliko kama hilo, basi, mimi naamini kwamba wale wanaotaka kuwa waaminifu kwa Mungu hawana budi kusimama kidete na kuuangalia ushahidi huu unaotolewa. Hapa tena, si suala la siku mbili; **ni suala la utii kwa Mungu**. Ni suala la kuamua iwapo tutakuwa waaminifu kwa kile asemacho Mungu na kumtii au iwapo tutageuka na kuzipa kisogo amri za Mungu na kuifuata njia nyingine.

Hebu na turudi nyuma na kuliangalia tena fungu lile la Danieli - fungu ambalo nabii yule alitabiri kwamba mamlaka fulani ingetokea na kubadili Sheria za Mungu zinazohusu majira. Zingatia kwamba Danieli anasema kwamba mamlaka hii ita"*azimu* kubadili majira na Sheria" (Danieli 7:25, mkazo umeongezwa). Ni jambo la kusisimua kwamba Biblia ingeweza kusema kwa njia kama ile. Je, kanisa lo lote au taasisi yo yote au mamlaka yo yote kweli inaweza kubadili amri ya Mungu, kama Mungu mwenyewe hajafanya badiliko hilo? Kwa kweli, la. Tunaweza kujaribu kuibadili Sheria ya Mungu. Tunaweza *kuazimu* kwamba tumekwisha kuibadili Sheria ya Mungu. Na hata tunaweza kuwapata watu wa kutufuata katika kutoitii Sheria ya Mungu. Lakini kwa kweli hatuwezi kubadili mojawapo ya amri za Mungu, au sivyo? Kanisa Katoliki linakiri kwamba hakuna mamlaka ya Biblia - hakuna fungu mahali po pote katika Maandiko - la kumwabudu Mungu siku ya Jumapili, lakini kwa vyo vyote vile kanisa hilo linadai kwamba limekwisha kufanya badiliko hilo.

# Kwa Nini Suala Hili ni la Maana Sana?

"Lakini kwa nini kuleta msukosuko huu juu ya jambo hili? mtu mmoja anauliza. "Kwa nini ni la maana sana?"

Ni la maana, kama tulivyoonyesha tayari, kwa sababu hoja yenyewe kwa kweli ni hii: "Ni nani tutakayemtumikia? Je, tutakuwa waaminifu kwa Mungu na kumtii yeye? Au, je, tutaitii ile mamlaka ambayo imeipa kisogo amri yake [Mungu] iliyo dhahiri?" Kwa kweli ni rahisi kama hivyo. Ni suala la kumtumikia na kumtii Mungu. Yesu alisema, "Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu" (Marko 7:7).

Tena kuna sababu nyingine inayolifanya suala hili kuwa la maana. Biblia inaonyesha kwamba kadiri tunavyokaribia zaidi na zaidi kuelekea mwisho wa historia ya ulimwengu huu, suala hili la utii kwa Mungu litajitokeza zaidi sana na kuwa la maana zaidi. Ufunuo 14 unatoa picha ya ujumbe wa mwisho wa Mungu kwa wanaume na wanawake kuwa utatangazwa kupitia angani na malaika watatu. Malaika hao ni mfano. Wanawakilisha ujumbe wa mwisho wa Mungu ambao unapelekwa na wanaume na wanawake ulimwenguni kote. Hebu, basi, na tuangalie kwa kifupi ujumbe huu wa aina tatu ambao Mungu ametupa hapa katika mwisho wa wakati kabla tu hajaja Yesu.

Ujumbe wa malaika wa kwanza ni wito wa kumwabudu Mungu Muumbaji. Kwa kweli, lugha yenyewe inatukumbusha sisi juu ya maneno yale yaliyotumika katika amri ya nne. Malaika wa kwanza asema hivi:

"Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji" (Ufunuo 14:7).

Vilevile, amri ya nne yatuambia sisi kumwabudu Mungu kwa sababu yeye ni Muumbaji wa vitu vyote mbinguni, duniani, na baharini. Yatuambia kwamba siku ya pekee ambayo Mungu ameitenga kwa ajili ya ibada ni siku ya saba ya juma - siku ya Sabato yake takatifu (angalia Kutoka 20:8-11).

Ujumbe wa malaika wa pili ni huu:

"Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake" (Ufunuo 14:8).

Babeli lilikuwa ni taifa katika Agano la Kale ambalo liliishambulia Israeli, yaani, watu wa Mungu, na kuwachukua mateka. Babeli lilikuwa ni taifa lililojaribu kuifutilia mbali ibada ya Mungu wa kweli wa mbinguni na mahali pake kuweka miungu ya kipagani. Na hivyo Babeli ikawa ishara iliyowakilisha majeshi yote yatakayowapinga watu wa Mungu katika siku za mwisho. Kwa hiyo malaika huyu wa pili anasema kwamba Babeli umeanguka kwa sababu umeyafanya mataifa yote ya dunia kunywa mvinyo ya uasherati wake, yaani, hiyo ni njia ya kusema kwamba majeshi yanayopigana na Mungu katika siku hizi za mwisho yatajaribu kumlazimisha kila mmoja kutoa utii wake kwa majeshi hayo kuliko kwa Mungu. Imewakilishwa kama "uasherati," au uzinzi. Kutokumtii Mungu kunaonyeshwa katika Biblia kama uzinzi wa kiroho. Mara hii tena, jambo hili lote linatufikisha kwenye hoja ya utii.

Mwisho, yule malaika wa tatu anatangaza hivi:

“Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo” (Ufunuo 14:9,10).

Maneno haya machache ni onyo muhimu kabisa ambalo Mungu amepata kulitoa katika Biblia. Anatuonya sisi dhidi ya kuisujudu mamlaka hii ambayo inapingana naye, naye anatuonya sisi tusipokee chapa yake. Mamlaka hii ni nani au ni kitu gani na alama yake ni alama gani?

Hii “mamlaka ya mnyama” ambayo sisi tunaonywa dhidi yake ni mamlaka ambayo picha yake inaonekana katika Ufunuo 13. Pale mamlaka fulani inawakilishwa ambayo inaipinga Sheria ya Mungu katika wakati huu wa mwisho, nayo inadai kwamba utii utolewe kwake na ulimwengu mzima badala ya kutolewa kwa Mungu. Na Ufunuo wasema hivi, “Na watu wote wakaao juu ya nchi **watamsujudu**, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo” (Ufunuo 13:8). Kinyume chake, Ufunuo 14:12 wasema, “Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao **wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu**.” Hivyo upande mmoja, tunalo kundi dogo la wale wanaoendelea kuwa waaminifu kwa Mungu na kwa Sheria yake. Na upande ule wa pili ni kundi kubwa sana la walimwengu watoao utii wao kwa mamlaka hii ambayo inajiweka mahali pa Mungu.

Chapa (alama) ya uwezo wa mamlaka hii ni nini? Je, unakumbuka kwamba tulipoyaangalia yale madondoo kutoka katika Kanisa Katoliki, tuliona kwamba kanisa hilo lilisonda kidole chake kwenye jaribio lake la kubadili siku ya Sabato ya Mungu toka Jumamosi kwenda Jumapili kuwa hiyo ndiyo “alama” ya mamlaka yake?

# Kusimama Njia Panda<br>Mahali pa Maana Sana

Ulimwengu mzima leo umesimama njia panda mahali pa maana sana. Sisi tunaamini kwamba Mtandao wetu huu wa Malaika Watatu unaotangazwa kwa Redio na Televisheni (Three Angels Broadcasting Network - **www.3abn.org**) upo kwa madhumuni ya kusaidia kuyapinga mambo ya udanganyifu ambayo Shetani anajaribu kuyatoa leo ulimwenguni kote kwa hila. Anawadanganya watu na mashirika ya kidini ya ulimwengu mzima ili wapate kumsujudu yeye kwa kuitunza sabato yake ya uongo badala ya Sabato Takatifu ya Mungu. Amewashawishi watu wenye dini na mashirika ya kidini kuiweka Jumapili, siku ya kwanza ya juma, mahali pa Sabato ya Mungu ya kweli, yaani, Jumamosi, siku ya saba ya juma.

Kama tulivyokwisha kusema mara kadhaa huko nyuma, suala sio tu Jumapili dhidi ya Jumamosi. Hoja yenyewe ni hii: Je, hivi mimi nataka kutoa utii wangu kwa taasisi za kidunia kwa kudharau maagizo ya Mungu na badala yake kuendelea kufuata mapokeo yaliyowekwa na wanadamu? Naamini kwamba kitabu hiki kidogo unachokisoma kimethibitisha bila ya kuwako mashaka yo yote kwamba kumwabudu

Mungu siku ya Jumapili msingi wake haukujengwa juu ya kitu cho chote zaidi ya mapokeo ya wanadamu kama yalivyowekwa na Kanisa Katoliki zamani sana kama karne ya nne hivi baada ya Yesu. Tuliona mapema kwamba mfumo huu wa upapa unatimiza barabara maelezo ya ile mamlaka iliyofichuliwa katika Danieli 7 na Ufunuo 13 na 14 - mamlaka itakayofanya jaribio la kubadili Sheria ya Mungu. (Zingatia kwamba mara kadhaa Ufunuo hutaja waziwazi utunzaji wa amri [kumi] kuwa ndiyo tabia inayowatambulisha watu wa Mungu katika siku hizi za mwisho. Angalia Ufunuo 12:17; 14:12.) **Maelezo mengi juu ya suala hili kama yalivyotolewa katika kitabu hiki kidogo si mapya**. **Yamejulikana na kufahamika kwenda nyuma sana katika siku zile za Martin Lutheri na za Matengenezo ya Kanisa**.

Lakini kile ambacho huenda hakijulikani kwa vizuri sana ni ile maana ya ile **sanamu** ya mamlaka hii. Ufunuo 14:9 husema juu ya "sanamu" ya mamlaka hii na kutuonya dhidi ya kuendelea kuisujudu hiyo pia. Hebu nitoe maelezo:

Ninapojiangalia katika kioo, najiona mimi mwenyewe - yaani, ninavyoonekana. Ile "sura" kwa kweli sio mimi; ni nakala inayonionyesha mimi nilivyo kwa ukamilifu. Sura ile katika kioo inadhibitiwa na kuongozwa nami; haifanyi lo lote kwa yenyewe. Ni sawasawa na sanamu ya mnyama iliyotajwa katika Ufunuo 14:9. Sanamu hiyo inadhibitiwa na mnyama yule mwenyewe. Mamlaka hii inapojaribu kuibadili Sabato ya Bwana ya siku ya saba, kama Danieli alivyotabiri (angalia Danieli 7:25), papo hapo sanamu ya mnyama inafanya vivyo hivyo bila kufikiri.

Tumeziona semi nyingi kutoka katika Kanisa Katoliki la Roma ambazo zinakiri waziwazi kufanyika kwa jitihada yake katika kuibadili Sheria ya Mungu pamoja na Sabato. Waprotestanti, kwa sababu hasa ya jina lao hilo, wanadai kuyapinga au kuyakataa - makosa yaliyofanywa na Kanisa Katoliki. Lakini kwa kuitunza Jumapili kama Sabato, jambo ambalo halitegemei kitu cho chote zaidi ya mapokeo ya Kikatoliki, Waprotestanti hao wamegeuka na kuwa sanamu ya mamlaka ile.

Mungu anasema kwamba wale wanaoipokea [wanaoikubali] sanamu hii au chapa (alama) ya mamlaka hii ya mnyama wa"takunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake" (Ufunuo 14:10).

Haya ni maneno mazito sana. Ni dhahiri, sisi hatutaki kuifuata mamlaka hii ya mnyama, wala sanamu yake, wala kuipokea chapa (alama) yake. Tunataka kuwa miongoni mwa wale ambao picha yao imeonyeshwa katika fungu la 12 - wale "wazishikao amri za Mungu" kwa uaminifu. Mojawapo la mafungu ya mwisho kabisa katika Biblia linasisitiza tena umuhimu wa kuendelea kuwa waaminifu kwa Mungu licha ya shinikizo lote ambalo Shetani anaweza kuliweka juu yetu. Ufunuo 22:14 husema, "**Heri wale wazishikao amri zake [Mungu], wawe na haki ya kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake**" (Toleo la Biblia la King James).

Waweza kushangaa. Je, kuna mtu ye yote aliye na alama ya mnyama hivi sasa? Je, hivi mimi tayari nimechelewa mno?

Jibu ni, Hapana. Hakuna ye yote aliye na alama ya mnyama leo. Mpaka hapo masuala haya yatakapowekwa wazi sana katika wakati wa mwisho na mtu atakapofanya uamuzi wake kwa kutumia akili yake kumfuata huyo mnyama katika suala hili la Jumapili na kuipinga Sabato ya Mungu, ndipo mtu awaye yote kama huyo atakapopokea alama ya kuogofya sana ambayo Mungu anatuonya sisi dhidi yake. Pambano kuu limekuwa likiendelea kati ya Kristo na Shetani kwa miaka 6,000 iliyopita. Pambano hilo

bado linaendelea leo. Pambano lenyewe ni juu ya roho zetu - nani atazidai kuwa zake? Je, tutatumia umilele pamoja na Kristo kule mbinguni au tutapotea milele?

Je, unaipata picha hiyo? Kadiri tunavyoikaribia zaidi na zaidi siku ya kuja kwake Yesu na ule mwisho wa dunia, ndivyo suala hili litakavyozidi kuwa ni moja ambalo linahusu uaminifu wetu kwa Mungu - kama litakavyodhihirishwa kwa vitendo kwa utii wetu kwake. Je, tutaitii amri yake ya kuitakasa Sabato ya siku ya saba au je, tutaipokea alama ya mamlaka inayoweka mapenzi yake mahali pa Mungu - kwa kuitii mamlaka yake ya kuibadili Sabato kwenda Jumapili, siku ya kwanza ya juma? Upande mmoja tunayo mamlaka inayodai kwamba watu wote waonyeshe utii wao kwake, kwa kutoijali Sheria ya Mungu, kisha waipokee alama yake. Upande mwingine ni wale wanaosisitiza kwamba watu waendelee kuwa waaminifu kwa Mungu na kuzishika amri zake - ikiwamo na Sabato ya siku ya saba ambayo ni amri ya nne. Hii ndiyo maana suala hili la Sabato ni la maana sana - na ndiyo sababu litazidi hata kuwa la maana zaidi tunapozidi kuukaribia mwisho wa ule wakati.

Mara moja tena, nataka kukazia kwamba sisi hatuna mashaka yo yote dhidi ya watu walio waaminifu au Wakristo wengine. Tunazungumza juu ya taasisi na mifumo na mashirika na misimamo wanayochukua. Tunazungumza juu ya kile lisemacho Neno la Mungu juu ya hali ilivyo na jinsi itakavyozidi kukua. Sisi tunaamini kwamba kuuangalia kwa karibu zaidi unabii wa Danieli na Ufunuo huonyesha kwamba mamlaka zinazompinga Mungu katika siku hizi za mwisho zitajaribu kuifutilia mbali Sabato Takatifu ya Mungu na kumlazimisha kila mtu kuitambua mamlaka ya siku ile iliyowekwa badala yake. Lakini kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo, hakuna mstari hata mmoja wa Maandiko unaoidhinisha badiliko la Sabato asilia ya Mungu ya siku ya saba kwenda katika siku nyingine iwayo yote. Ufunuo unatabiri kwamba **suala hili la Sabato litakuwa ndicho kipimo sahihi** kwa ulimwengu mzima - na suala lenyewe ni hili tu: Je, hivi tutamtii Mungu au hatutamtii?

Kipindi kifupi cha miaka sitini au sabini au themanini tunachokitumia katika sayari hii iitwayo Dunia ni kipindi tu cha kupimwa ambacho katika hicho sisi tunaamua wapi tunataka kutumia umilele wetu. Bwana ametuumba sisi tukiwa na uhuru wa kuchagua. Tunaweza kuchagua; tunaweza kuamua sisi wenyewe. Tunaweza kumwomba Mungu atusamehe dhambi zetu na tunaweza kumwomba tumtumikie. Au tunaweza kumtumikia yule mwovu. Hakuna kusimama katikati.

Mtu mmoja anaweza kuuliza, "Itakuwaje kwa mama yangu? Alikuwa mwanamke Mkristo mwema sana, lakini hakuitunza kabisa Sabato ya siku ya saba. Je, atapotea?

Waweza kuhakikishiwa kwamba hakuna mtu ye yote atakayepotea kwa bahati mbaya. Mungu anatuhesabu kwamba tunawajibika tu kwa kile ambacho tumekuwa na nafasi nzuri ya kujifunza na kukielewa. Biblia yasema hivi, "**Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi**" (Yakobo 4:17). Kumbuka tafsiri ya Biblia ya dhambi - "**dhambi ni uvunjaji wa Sheria**" (1 Yohana 3:4, AJKK/HN). Kutoitii Sheria ya Mungu kwa makusudi ni dhambi. Mara hii tena, weka mawazoni mwako kwamba suala hili halihusu sana siku kama linavyohusu utii wetu kwa Mungu. Linahusu kumpenda na kumtii Mungu kwa uwezo wetu wote. Hayo ndiyo yote tuwezayo kufanya. Tunapofanya makosa, huku tukiwa wanyofu mioyoni mwetu, kwa sababu sisi hatujui lililo jema zaidi ya hilo, damu ya Mungu inatufunika. Hatuwezi kufanya matendo mema ili kwenda mbinguni. Tunaokolewa kwa neema na kwa neema peke yake - si

kwa utunzaji wetu wa Sabato au kwa tendo letu jingine lo lote la utii. Tunamtii Mungu kwa sababu tunampenda. Yesu alisema, “Mkinipenda, mtazishika amri zangu” (Yohana 14:15).

La, mama yako hatapotea kwa sababu yeye hakuweza kukitii kitu ambacho alikuwa hakielewi. Tunaweza kupotea tu wakati ule sisi wenyewe tunapochagua kumkataa Mungu na kusimama upande wa Shetani.

# Amri za Jumapili na Siku za Usoni

Dunia kwa haraka sana inakaribia mwisho wake. Shetani anajua kwamba anao wakati mchache tu, naye “kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze” (1 Petro 5:8). Hivi sasa anapigana vita na watakatifu wa Mungu walio waaminifu asivyopata kupigana nao kamwe huko nyuma. Amedhamiria kujipatia utii kutoka kwa kila mmoja kwa kadiri awezavyo. Na sisi wanadamu tunacheza na kujiweka kabisa mikononi mwake. Hebu nitoe maelezo.

Leo katika nchi ya Amerika kuna vuguvugu la kidini linalofanya mambo yake kichini-chini ili kuifanya Jumapili iwe siku takatifu. Kwa kweli, jitihada hii imekuwa ikiendelea kwa zaidi ya miaka mia tatu. Ilianza kwa Wapyuritani (Puritans) waliofanya makao yao kule New England. Waliamini kwamba wao walikuwa wakianzisha ufalme wa Mungu hapa duniani. Kwa hiyo walitunga sheria zilizolazimisha desturi za kidini, pamoja na kuiadhimisha Jumapili kama wao walivyoamini kwamba mambo hayo yangepaswa kufanywa vile. Kwa mfano, waliwakataza hata wale waliooana kubusiana katika siku ya Jumapili. Ni kweli, waliacha pia kufanya kazi Jumapili, wakichukua agizo hilo moja kwa moja kutoka katika amri ya nne. Majimbo fulani ya Amerika bado yanalazimisha sheria hizo. Kwa mfano, katika Illinois, wauzaji wa magari hawaruhusiwi kuuza magari yao siku ya Jumapili. Orodha ya shughuli zilizopigwa marufuku inatofautiana toka jimbo hadi jimbo, na hata serikali za mitaa zinaweza kutunga sera zake katika mambo mengi. Kwa mfano, katika jumuia ambayo mimi naishi ndani yake, watoto wa shule za serikali wanaruhusiwa kufanya mazoezi ya riadha ya shule katika siku ya Jumamosi, ambayo si siku ya kawaida ya shule, lakini hawaruhusiwi kufanya mazoezi yaliyopangwa ya shule katika siku ya Jumapili.

Nyingi miongoni mwa sheria hizi za kidini na wale wanaozipigia debe huonekana kana kwamba zinachochewa kisiasa. Panaonekana kama ipo juhudi ya kuwapigia debe Wakristo kugombea vyeo vya serikali. Viongozi wengi wa kidini wanawatia moyo Wakristo kugombea vyeo katika serikali za mitaa, serikali za majimbo, na ofisi za muungano. Je, ni kwa kusudi gani? Jibu linaonekana dhahiri kwangu - ni kuibadilisha serikali.

Basi, hilo halionekana kama ni wazo baya mwanzoni. “Kwa vyo vyote vile,” Wakristo wengi wanasema siku hizi, “angalia mifumo ya shule zetu nyingi ilivyovurugika. Mungu ameondolewa kabisa kutoka katika shule hizo. Nadharia ya kuibuka vitu vyenyewe inafundishwa badala ya uumbaji. Waalimu hawaruhusiwi kuanza siku ya shule kwa maombi. Amri Kumi zimeondolewa kutoka katika kuta za madarasa. Kila mtu anaweza kuona matokeo ya mambo haya yote ambayo yanazidi kuongezeka ya kuwa ni mojawapo ya sababu zinazoonyesha kwa nini sisi tunayo matatizo mengi sana shuleni leo - kila kitu kuanzia masomo duni hadi kuuawa shuleni kwa kupigwa risasi.”

Kwa hiyo sababu inayowafanya viongozi wengi wa dini kuwashurutisha Wakristo kugombea vyeo serikalini, pamoja na katika bodi za shule, ni kuweza tu kujipatia uwingi ili kuweza kubadili sheria na sera. Makusudi yao huenda yakawa mazuri, lakini mara tu hilo linapotokea, uwezekano wa kuyatumia vibaya unaonekana kila mahali. Mabadiliko yanakuwa rahisi kufanya. Yale yote ambayo hayana budi kutokea ni kuzipigia kura sheria mpya zilizojengwa juu ya Biblia.

Kwa mfano, kama idadi ya kutosha ingekuwamo katika bodi za shule za mahali mahali na endapo wangekuwa na mamlaka ya kufanya hivyo, basi, wangeweza kubatilisha marufuku iliyowekwa dhidi ya maombi shuleni, wangezirudisha Amri Kumi madarasani, wangeanza kufundisha Uumbaji. Jambo hilo lisingeweza kupunguza kwa ghafula uhalifu na ukatili ... na wanafunzi wote wasingeanza kumpenda Yesu na kurudi kanisani. Hebu fikiria tu iwapo Mkristo mwenye ajenda kama hiyo angekuwa Rais wa Marekani! Au, ingekuwaje kama muungano wa Wakristo kama hao ungekuwa na wajumbe wa kutosha na kuweza kuwashawishi kweli kweli viongozi wa serikali. Je, kuna uwezekano kwamba mambo haya tayari yanaendelea kutokea? Wengine wanaweza kusema, "Kama jibu ni ndiyo, kuna nini, basi? Hayo yanasikika kuwa ni mazuri kuliko yale yaliyopo na yanayoendelea hivi sasa."

Lakini mimi naliona tatizo kubwa kuwa lipo kutokana na mawazo ya aina hii. Mama yangu alizoea kuniambia hivi, "Mtu aliyeshawishiwa kinyume na mapenzi yake, bado ana maoni yake yale yale." Kusema wazi, **serikali za mitaa**, **serikali za majimbo**, **na serikali ya muungano zinaweza kupitisha sheria zote watakazo za maadili**, **wala hilo halitalibadilisha tatizo la dhambi iliyo ndani ya moyo wa mwanadamu**. **Ni Yesu peke yake awezaye kufanya hilo**!

Viongozi wengi wa dini wanaweza kuwa na maana nzuri; mimi kwa hakika siwezi kuyahukumu makusudi yaliyo mioyoni mwao. Lakini dini haitakiwi kulazimishwa juu ya watu kwa kutunga sheria zilizokusudiwa kulazimisha kwa kutumia nguvu itikadi za kimaadili. Sisi hilo tunalijua tayari. Tumekwisha kuona jambo kama hilo likitokea katika historia wakati wa Zama za Giza. Mamilioni mengi ya watu waliuawa kwa sababu uongozi wa kanisa ulikuwa na nguvu nyingi kuliko uongozi wa kidunia. Utawala wa kanisa na serikali vikaunganishwa pamoja. Kama matokeo ya mateso yale, watu walitimua mbio na kwenda Marekani ambako Katiba ilikuwa imewekwa ambayo ilitoa uhakikisho kwamba mateso hayatatokea tena.

Jambo hili halikutokea zamani tu. Leo wapo viongozi wanaoendelea kusisitiza muungano wa kanisa na serikali. Charles Malik, Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Balozi katika nchi ya Marekani na Mhadhiri Mwalikwa pale Harvard, alisema hivi:

"Tumaini la pekee kwa ulimwengu wa magharibi limo katika muungano kati ya Kanisa Katoliki la Roma, ambalo mvuto wake kwa kawaida una nguvu nyingi sana ya kuongoza, kudhibiti, na kuiunganisha Ulaya na Kanisa la Mashariki la Othodoksi (Eastern Orthodox Church). Roma ni lazima iungane na Uothodoksi wa Mashariki, kwa sababu Kanisa Othodoksi la Mashariki linatawala sehemu ya magharibi ya Mashariki ya Kati, [upande wa mashariki wa Mediterania], na kama wasipouimarisha udhibiti ule, basi, Uislamu utatembea na kuingia Ulaya. Dini ya Kiislamu ni ya kisiasa. Basi, tumaini la pekee kwa ulimwengu wa magharibi linategemea muungano wa Ulaya chini ya udhibiti wa Papa. Na halafu ndipo Wakristo wote wa Kiprotestanti ulimwenguni kote

watalazimishwa kumtii Papa ili tupate kuwa na ulimwengu wa Kikristo uliounganishwa pamoja."

Shetani anashughulika kwa jumla juu ya kudhibiti. Haileti tofauti yo yote kwake kama anawatumia viongozi wa kanisa au wakuu wa serikali za kidunia. Amefanikiwa sana katika vipindi vilivyopita kwa kuchanganya kanisa na serikali, na hilo ndilo hasa analojaribu kulitimiza tena katika siku zetu.

**Mimi naamini kwamba katika muda mfupi sana ujao tutaona Jumapili ikitukuzwa kama siku ya ibada na juhudi ikifanywa na kanisa na serikali kupitisha amri ya Jumapili kitaifa na kutangaza kwamba kama kawaida shughuli za kazi na biashara Jumapili ni lazima zifungwe**. Mawazo nyuma ya vuguvugu hilo ni haya tu: maadili ya jamii yetu yanamomonyoka kwa haraka sana, hasa miongoni mwa vijana, viongozi wetu wa kesho. Sisi sote tunajua kwamba Mungu anaonekana kana kwamba anaondoa mibaraka yake kutoka Marekani kwa sababu ya uasi wetu kwake. Kwa hiyo watu wanawaza kwamba kama taifa, sisi ni lazima tufanye kitu fulani kwa ukali kumwonyesha Mungu ya kwamba sisi bado ni Wakristo. Wao wanafikiri kwamba endapo tutapitisha amri ya Jumapili kwa taifa zima, basi, taifa letu mara moja tena litakuwa likimkaribisha Roho Mtakatifu wa Mungu kurudi katika serikali yetu, nasi tutakuwa tena taifa la kiroho zaidi.

Hizi ndizo sababu zitakazotumika kuhalalisha sheria zitakazosisitiza utunzaji wa Jumapili. Idadi yo yote ya matukio ingeweza kuharakisha mno sheria hii ya Jumapili kitaifa - yaani, maafa kama vile Kituo cha Biashara cha Ulimwengu kilichoharibiwa. Angalia jinsi watu walivyoingiwa na jazba kwa tukio hili la karibuni: waliingiwa na hofu kuu, bei za mafuta zilipanda juu, na mara moja pakawa na vipindi vya maombi na wito kwa taifa hili kumrudia Mungu. Kurejeshwa kwa amri za Jumapili ni nyongeza ya kawaida kwa mpangilio wa matukio yanayotabiriwa kutokea baadaye.

Na ngoja nikuambie kwamba naamini hatujapata kuona kitu cho chote bado! Taifa hili kubwa litakapoanza kuwakandamiza watu - kwa njia ya sheria zilizotungwa Bungeni - kuhusu siku wanayopaswa kumwabudu Mungu, hapo ndipo tatakapoona wakati wa taabu usiopata kuwako huko nyuma. Kwa kweli, Marekani itakapopitisha amri ya Jumapili kwa taifa zima na kuwakataza watu kufanya kazi na biashara zao kama kawaida siku ya Jumapili, ndipo tutakapomwona Mungu akimwondoa Roho wake. Kwa nini? Kwa sababu badala ya kuonyesha utii wetu kwa Mungu kwa kumwabudu katika Sabato yake Takatifu ya siku ya saba, badala yake tutakuwa tukitoa ahadi zetu kumtii Shetani kwa kuiheshimu Jumapili, sabato yake ya uongo. Hebu niweze kurudia? Suala hili halihusu siku tu, linahusu nani ambaye mimi nitamtumikia.

Ukiangalia kwa karibu zaidi mpangilio huu wa matukio yanayotarajiwa, utagundua kwamba si upapa ambao moja kwa moja utazipitisha sheria hizo za kidini Bungeni. Kwa kweli, leo kwa sehemu kubwa ni Waprotestanti - ambao imani yao imejengwa juu ya Biblia, na Biblia peke yake - hao ndio wanaounda muungano wa kidini unaojaribu kuwashawishi viongozi wa kisiasa. Hata hivyo, Shetani anayatumia makundi kama hayo kama chambo katika jaribio lake la kuisimika serikali yake. Waprotestanti, bila kutumia akili wanatekeleza maagizo ya mamlaka ya yule mnyama, wanageuka na kuwa sanamu ya mamlaka hiyo. Hebu na tuangalie mara moja tena Ufunuo 14:9: "Malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa (alama) yake katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu

ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake."

Swali: Mtu anamsujuduje huyo mnyama na sanamu yake? Jibu: Kwa kumdharau Mungu na amri zake - ikiwamo na ile ya nne - huku akiwa anajua analofanya na kuendelea kuitunza sabato ya uongo badala ya Sabato ya Mungu ya siku ya saba.

Kwa sasa, unaweza kuwa unashangaa kwa nini mimi nina hakika kabisa kwamba itakuwako amri ya Jumapili kwa taifa zima ambayo itatekelezwa na serikali ya Marekani kabla Yesu hajaja. Hebu na tusome Ufunuo 13:3. "**Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule**." Mamlaka hii ni dhahiri kwamba ni ile ambayo mamlaka yake ulimwengu mzima - yaani, kila taifa - unayatii. Je, mpaka hapo kuna kitu kinginecho chote ambacho ulimwengu mzima unakubaliana nacho kiasi cha kufuata uongozi wa mamlaka hiyo? Baada ya kusafiri sana duniani, ni maoni yangu kwamba utakatifu wa Jumapili na kufunga kazi na biashara siku ile ni mojawapo ya mambo machache sana ambayo karibu ulimwengu mzima unakubaliana nayo.

# Je, Yatupasa Kufanya Nini?

Hebu na tusome fungu jingine - Ufunuo 13:17. "Mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa (alama) ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake." Nadhani tunaweza kukubaliana kwamba kama huu ni utabiri wa kweli uliomo katika Neno la Mungu wa kupiga marufuku biashara, basi, hapana budi kutakuwa na kitu fulani ambacho ulimwengu utaweza kutumia kuamua ni nani ataweza kununua na kuuza. Kitakuwa ni kitu fulani kitakachoashiria utii wetu tulio nao kwa mamlaka hii. Hebu na tuseme kwamba amri ya Jumapili ingepitishwa ili kupiga marufuku watu wasifanye kazi au wasinunue au wasiuze siku ya Jumapili. Kungetokea nini kama mtu fulani asingeitii amri hiyo, bali badala yake angemwabudu Mungu katika Sabato ya siku ya saba? Vipi kama angefungua duka lake Jumapili kama kawaida licha ya kuwapo amri hiyo. Unadhani kwamba biashara ile ingefungwa?

Ndiyo, utakatifu wa Jumapili ungeweza kuwa ndiyo ile alama iliyosemwa katika Ufunuo 13 na 14. Kumbuka, alama hii itakuwa ni kitu fulani kinachoadhimishwa kwa kiwango cha juu sana kiasi kwamba ulimwengu mzima utajua habari zake. Na ili alama hii iweze kulazimishwa kisheria kwa kupiga marufuku kununua na kuuza, basi, ni lazima patakuwa na sheria zitakazopitishwa Bungeni. Bado hatujafika hapo, lakini naamini kwamba wakati huo, uliotabiriwa katika Neno la Mungu, unatunyemelea kwa haraka sana.

Je, tusingetoa nadhiri ya utii wetu leo kwa Mungu Muumbaji mkuu wa malimwengu yote na kuanza kujiandaa sasa kuzishika amri zake zote?

Ni Mungu mwenyewe aliyeiandika amri ya nne juu ya mbao za mawe, akituamuru sisi kuitakasa Sabato ya siku ya saba. Katika Isaya, Mungu anatuambia kwamba tutaitunza Sabato milele na milele kule mbinguni. "Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, na **sabato hata sabato**, wanadamu **wote** watakuja kuabudu mbele zangu, asema BWANA" (Isaya 66:23).

Swali langu kwako wewe ni hili: Kwa nini Mkristo asitake kumheshimu Mungu kwa kuitunza Sabato yake sasa kama maandalizi ya kuitunza mbinguni milele na milele? Wakristo hawaoni kwamba wanaweza kuziacha amri zile nyingine tisa za Mungu mpaka

hapo watakapoanza kuzitunza kule mbinguni. Kwa kweli, makanisa yote ya Kikristo yanafundisha kwamba kama tunaua, tunaiba, tunazini sasa, basi, tutapotea wala hatutakwenda kamwe mbinguni - isipokuwa kama tutaziungama dhambi hizi na, kwa neema yake Mungu, kuacha kuzifanya. Je, unaweza kuwaza kwa kutumia sababu iyo hiyo, wanayotoa Wakristo ili wasiendelee kuishi katika dhambi hizi, kuhusiana na uvunjaji wa amri ya nne?

Hata hivyo, Wakristo wengi wanajaribu kutoa sababu zao kwamba si jambo la maana kuitunza amri ya Mungu ile ya nne. Je, kuna Mkristo awaye yote ambaye angethubutu kusema hivi: "Ni sawa kabisa kuwaua watu kwa sababu hiyo si amri ya maana sana"? Bila shaka, la! Sisi sote tunakubali kwamba ni kosa kuiba. Sisi sote tunakubali kwamba ni kosa kuzini.

Je, unaweza kuona jinsi Shetani anavyowadanganya wanadamu wote na jinsi anavyopanga kwamba ulimwengu mzima hivi sasa utoe nadhiri ya utii wao kwake kwa kuitukuza sana Jumapili kama alama ya utii kwake?

Kwa kufunga, hebu nikuulize swali hili: Tunaamuaje kwamba kweli ni nini?

Je, tunaitambua kweli kwa kufuata kura ya wengi? Mambo mengi tunayaamua kwa kupiga kura na halafu kufuata kura ya wengi. Lakini hatuwezi kufanya hivyo kuhusiana na kweli. Hatuamui kuwa hii ni kweli kwa kufuata kura ya wengi. Kweli ni kweli hata kama hakuna aliye mkweli. Na kosa ni kosa, hata kama kila mmoja ana makosa. Katika mambo ya kiroho, kweli ni kile asemacho Mungu katika Neno lake. Siyo kile *tunachokiamini* kuwa ni kweli. Si kile tunachotaka sisi kiwe kweli. Si kile watu wengi *wanachokubaliana* kuwa ni kweli. **Ni kile Mungu asemacho kuwa ni kweli!**

Je, ni jambo la maana kweli - yaani, suala hili la Sabato ya Mungu ya siku ya saba? La, endapo ni suala tu la Jumamosi dhidi ya Jumapili. Lakini kama ni suala la Yesu dhidi ya nafsi zetu - yaani, Njia yake au njia yetu - basi, jambo hilo ni la maana, au sivyo? Kama ni suala la utii kwa Mungu au utii kwa mamlaka zile zinazompinga Mungu, basi, jambo hilo ni la maana, au sivyo? Yesu anasema, "Mkinipenda, mtazishika amri zangu" (Yohana 14:15). Hoja yenyewe, basi, si juu ya siku moja au siku nyingine. **Hoja yenyewe ni upendo na utii wetu**. Yesu ametuambia kuhusu mapenzi yake kuhusiana na Sabato. Je, hivi tunampenda kiasi cha kutosha kuweza kumtii?

Ni ombi langu kwamba kila mmoja wetu atakuwa miongoni mwa wale wanaozishika amri zake na kuwa na "haki ya kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake" (Ufunuo 22:14).

[Kwa maelezo zaidi juu ya somo hili, tafadhali andika kwa:

3 Angels Broadcasting Network,
P.O. Box 220,
West Frankfort, IL 62896
**www.3abn.org**].

Mtunzi: Danny Shelton.
Mfasiri: M. Mwamalumbili.